# Maji kwa ajili ya watu na mazingira katika eneo-bonde la Mto Wami

Kuwepo kwa maji safi na ya kutosha, ardhi yenye rutuba na vijiji vyenye maendeleo kwa wakazi wapatao milioni 1.8 wa eneo-bonde la mto Wami, kunategemea sana juhudi za sasa za utunzaji wa vyanzo vya maji na mazingira (ikiwemo misitu).

O Changamoto zilizopo katika vijiji vya eneo-bonde hili ni pamoja na:

- Upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo mbalimbali kwa wakati muafaka kutosheleza mahitaji yetu
- Kuhifadhi na kutunza vyanzo vya maji na mazingira ili kuwa endelevu.
- Kufuata kanuni za usafi wa mazingira kwa ajili ya afya ya jamii.



*Sehemu ya mto Wami katika maeneo ya Mtibwa*

Hivyo jamii inahitaji kushirikiana na kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha kwamba changamoto zilizopo zinashughulikiwa. Ofisi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu na Tanzania Coastal Management Partnership (TCMP) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika bonde waliweza kukabiliana na baadhi ya changamoto hizo kutokana na ufadhili uliotoka kwa muungano wa Wadau wa Maji na Maendeleo (WADA). Mambo muhimu yaliyoonekana katila utekelezaji wa mradi huo ni kama ifuatavyo.

### *Elimu ya Afya Mashuleni*

Shule nyingi zinazojengwa zimekuwa hazina miundombinu mizuri ya vyoo pamoja na uhaba wa maji kwa wanafunzi na walimu. Ujenzi wa vyoo mashuleni na katika maeneo ya makazi ya watu wengi ulifanyika katika vijiji vya Dumila, Msowero, Madizini, Hale na Miono, ili maeneo mengine yaweze kuiga. Kuna shule ambazo zilikaribia kufungwa kutokana na ukosefu wa vyoo. Aidha viongozi wa vijiji na kamati za maji,



*Choo kilichojengwa vizuri kitawaepusha watoto kuondokana na magonjwa ikiwa tu tabia na mazoea ya kunawa mikono kila baada ya kutoka chooni vitapewa umuhimu unaostahili*

walipewa mafunzo kuhusu Elimu ya afya na umuhimu wa kunawa mikono. Hivyo kuna umuhimu wa kueneza elimu ya afya katika maeneo mengine ya Bonde la Mto Wami.

Mradi wa kuvuna maji ya mvua ulijengwa katika kijiji cha Hale, ili kuwezesha upatikanaji wa maji safi na ya kutosha katika shule mojawapo ya sekondari. Hivyo, umuhimu wa upatikanaji wa maji siyo tu mashuleni bali ni pia katika vijiji kwa kutumia teknolojia rahisi.

### *Tathmini ya mahitaji ya Maji kwa ajili ya watu na Mazingira*

Sehemu nyingine ya mradi iliunda timu ya wataalam washauri wa fani mbalimbali mwezi Aprili 2007, ambao walifanya tathmini ya mahitaji ya maji kwa ajili ya mazingira na watu. Timu hiyo ilikusanya takwimu/taarifa mbali mbali katika mto Wami ili kuzifanyia uchambuzi wa kina kwa kusudi la kufahamu hali halisi ya afya ya mto na rasilimali zilizopo na uwezo wake wa kukidhi mahitaji mbali mbali ya watu na mazingira. Lengo lilikuwa ni pamoja na:

- kuwa na takwimu/taarifa za kutosha kuhusu wingi na ubora wa maji katika mto Wami (water resources database)
- Kujua matumizi halisi ya maji katika mto (water use database)
- Kufahamu mahitaji halisi ya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali ili kuwezesha mipango na ugawaji wa haki na uwazi

Kwa ujumla, takwimu za awali zilionyesha kwamba

The Water and Development Alliance (WADA) is a collaboration between the Coca-Cola System (including corporate, foundations, and bottling partners) and USAID to improve water resource management and expand access to improved drinking water and sanitation services for poor and marginalized people in developing countries.

mto Wami bado uko katika hali nzuri na hivyo tunahitaji kuendelea kuweka mikakati ya kuutunza.
Upanuzi wa mashamba pamoja na viwanda unatakiwa uende sambamba na utunzaji wa rasilimali ya maji pamoja na kupunguza uchafuzi ili kuzuia upungufu wa maji na migogoro itakayojitokeza.

***Utunzaji wa Ardhi***

Baadhi ya vijiji vimehamasika katika utunzaji wa ardhi kwa kuhifadhi miti na hivyo kusaidia kupunguza mmomonyoko wa udongo ambayo ni njia mojawapo ya kuhifadhi maji chini ya ardhi. Miti husaidia siyo tu katika hifadhi ya vyanzo vya maji bali pia katika ujenzi, nishati na kivuli. Mpango wa upandaji miti na vitalu vya miche, ulipokelewa vyema na wananchi, hivyo ni mfano mzuri wa kuigwa. Hata hivyo kazi zaidi zinahitajika kufanyika katika Bonde.



***Wakulima na wanavijiji wako mstari wa mbele katika kuhifadhi maeneo yao lakini msukumo zaidi unahitajika***

***Kuhifadhi Rasilimali ya Maji na Mazingira***

Kilimo cha umwagiliaji mkubwa na shughuli za Viwanda huzalisha majitaka ambayo humwagwa kwenye mito na kuharibu ubora wa maji yake. Hali hii inahatarisha afya za wananchi pamoja na viumbe hai vya majini. Hivyo wataalamu kwa kushirikiana na Viwanda vya Mtibwa na Kigombe wanatayarisha mpango wa kupunguza matumizi ya maji pamoja na uchafuzi wa vyanzo vya maji. Uhamasishaji wa makampuni mengine kuiga mfano huu ni muhimu ili kuifadhi rasilimali zetu za maji na usafi wa mazingira.



***Viwanda vinaongeza tija kutokana na ongezeko la uwezo wa uzalishaji na kupunguza uchafuzi unaosababishwa na utupaji holela wa taka hatari***

***Mpango wa ufuatiliaji***

Juhudi zinahitaika katika kuendeleza huduma zilizopo kuwa endelevu na kupanuliwa katika maeneo yafuatayo:

- Kujenga vyoo na miradi ya maji mashuleni na maeneo mbalimbali vijijini
- Kuimarisha mafunzo ya usafi wa mazingira na kujenga miradi ya maonyesho vijijini
- Mashamba makubwa ya miwa na katani yanatakiwa kuchukua hatua za kuzuia/kupunguza uchafuzi wa vyanzo vya maji
- Viongozi wa Serikali, Vyama vya siasa na wadau wengine wanatakiwa kuhamasisha katika upandaji miti na utunzaji wa ardhi
- Matokeo ya awali ya tathmini ya mahitaji ya maji kwa ajili ya watu na mazingira katika Mto yanaiwezesha Ofisi ya Maji Bonde la Wami/ Ruvu kuimarisha takwimu zake kuhusu ugawaji / matumizi bora ya maji katika mto huo

Aidha matokeo hayo ya awali yanaweza kusambazwa kwa wadau mbalimbali wakiwemo wananchi kwa malengo tofauti ikiwemo kuzuia migogoro ya maji. Elimu hii inaweza kuingizwa kwenye mitaala ya shule.

Utekelezaji wa Programu hii katika mto Wami kuanzia ufukwe wa bahari hadi mwanzo wa mto wenyewe, umefanikiwa kutokana na mchango wa fedha kutoka Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), USAID Tanzania na Taasisi ya Coca -Cola Afrika na Coca - Cola Atlanta zikiwa ni sehemu ya WADA.

Washirika mahsusi wa programu hii ni pamoja na: Kituo cha Hifadhi ya Mazingira ya Pwani ya Chuo Kikuu cha Kisiwa cha Rhode kilichoko Marekani kupitia Taasisi ya Menejimenti ya Hifadhi ya Ukanda wa Pwani Tanzania (TCMP), Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Florida kilichoko Marekani na World Vision. Washirika wengine ni Taasisi isiyo ya kiserikali ya Afya na Usafi wa Mazingira (Tanzania Health, Environment and Sanitation Association (THESA)), Ofisi ya Maji Bonde la Wami/ Ruvu Kampuni ya Bonite Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa na TPC na Kiwanda cha Mkonge cha Kigombe pamoja na kamati za maji za vijiji husika.

***Kwa Maelezo zaidi wasiliana na***

Bwana Julius Sarmett kutoka Ofisi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu, S. L. P. 826, Morogoro. Simu: 255-23-261-4748. barua pepe: juliussarmett@yahoo.com

Bibi. Appa Mandari, Mratibu wa Programu kutoka Tanzania Coastal Management Partnership, Simu. (255-22) 278-0520. Barua pepe:apmandari@yahoo.com. Old Bagamoyo Road, Mikocheni B, Plot 390, P.O. Box. 71686, Dar es Salaam, Tanzania.

Bwana Donald Robadue na James Tobey, Coastal Resources Center, Chuo kikuu cha Rhode Island. Narragansett, RI, USA. Simu: 401-874-6224. Barua pepe: robadue@gso.uri.edu, tobey@crc.uri.edu